
@Kalamu_Na_Maisha
Utaniponza
NORAH
Kalamu Na Maisha
Na;- Mtengeleka, Ramadhani, S
+255 675 529 285

# *UTANIPONZA NORAH*

*Na;- Mtengeleka, Ramadhani. S*

*Phone no;- +255 675 529 285 / +255 685 691 690*

*Barua Pepe;- ramadhanimtengeleka@gmail.com*

## *SURA YA KWANZA..(01).*

Marco.. naam..‼ Hili ndilo lilikuwa ni jina langu halisi nililopatiwa na wazazi wangu. Katika familia yetu, nilibahatika kuzaliwa kama mtoro wa pili katika uzao wa watoto takriban watano wa familia ya Mzee Kasenga David. Ni nani ambaye hakuwa akilifahamu jina langu tangu nilipokuwa nikisoma Shule ya Msingi Kiwanja Cha Ndege..?? ama ni nani aliyekuwa hajazisikia habari zangu pindi nilipokuwa nikisoma Shule ya Sekondari ya Image..? Kila mtu, vijana kwa wazee, pengine hadi watoto, walikuwa wakinitambua vema kwa jinsi jina langu likisikika vema kila kona kutokana na uwezo wangu wa juu wa kucheza soka...hasa katika nafasi yangu ya mlinda lango.

Nilikuwa napendwa sana na watu, kila nilikopita basi niliitwa na kusimamishwa na watu kunipa pongezi. Nilibarikiwa kipaji safi cha soka na jambo la kushukuru ni kuwa kipaji changu kilionekana mapema sana, na kuwashangaza wengi.

Nilibahatika kufanya majaribio katika nyakati tofauti na katika timu tofauti, zilizokuwa zikipatikana ndani na nje ya mji mkuu wa Tanzania, Dodoma. Bahati mbaya, nilikuwa nikikwamishwa na mambo kadhaa ambayo pengine yalichelewsha kidogo suala la mimi kuanza kucheza soka katika ngazi za juu. Moja, lilikuwa ni suala la umri, maana nilikuwa nikidaka katika mashindano mbalimbali angali nikiwa kijana ambaye sijajitosheleza kiumri kuweza ama kusajiliwa na timu kubwa au kujikita zaidi kwenye mazoezi ya nguvu.

Pia, lilikuwepo suala la elimu. Hili mara nyingi silihesabu sana kama kikwazo mojawapo kilichofanya nisitambe mapema katika medani ya soka, kwa maana walionisomesha, yaani wazazi wangu, hakika walikuwa na lengo bora la kuniandaa kwa maisha yangu ya baadae. Japo, haibadili ukweli kuwa, nilitumia muda mrefu sana katika masomo hadi nilipohitimu Elimu ya juu kabisa ya chuo. Kuanzia hapo, wazazi hawakunikataza tena kucheza soka, nami sikutaka tena kurudi nyuma. Nikauweka mchezo huu moyoni, nao ukaniweka juu mbele za watu.

*. *. *.

Siku moja, miaka mingi baadae, nilikuwa nimesimama katikati ya mstari wa goli. Jua lilikuwa likipiga kiasi na kutufanya wachezaji tutokwe na jasho, ambalo pia lililetwa na shughuli pevu iliyokuwa ikiendelea uwanjani. Muda huo, nilikuwa nikitazamana uso kwa uso na moja kati ya wachezaji wa nafasi ya ushambuliaji waliokuwa wakitamba zaidi nchini, aliyekuwa akifahamika kwa jina la Shaban Mlope. Baina yetu, uliwekwa mpira katika kituo cha kupiga penati. Nilimtazama mwamuzi akiwatuliza wachezaji wengine waliosimama nje kidogo ya eneo la kumi na nane. Halafu nikatazama tena uso wa Mlope, uliokuwa umatota jasho na mishipia iliyochachamaa..!!

Kama kawaida yangu, mara zote nilipokuwa katika majukukumu yangu, hasa kunako suala la penalti, basi kwanza lazima nishushe pumzi nene ili kutuliza mapigo yangu ya moyo kama itatokea yanaenda kasi. Halafu niliutazama mpira kwa umakini kusubiri upigwa.

"Naam, mpenzi mtazamaji..!! Mwamuzi anapuliza kipyenga kuruhusu Shaban Mlope apige mpira. Anakwenda sasa...anapiga kuleeeee...!!! Anaokoa pale golikipa wa Wajenzi FC, Marco David...!!". Nilichupa kwa nguvu kuruka na kuupangua mpira uliopigwa kwa nguvu, kisha nikaanguka chini huku nikiutazama jinsi ulivyokuwa ukiambaa taratibu na kuvuka mstari kando ya goli na kutoka nje.

Haikuwa mara yangu ya kwanza kuokoa penalti. Nilifanya hivyo mara kwa mara katika historia yangu katika mchezo wa soka. Wachezaji wenzangu walikimbia haraka na kuja kunipa heko, mchezo ukapata kuendelea kama kawaida.

Siku hiyo, mechi iliisha pasina mshindi kupatikana baada ya kutoka sare ya 0- 0 dhidi ya timu ya JKT Tanzania. Nikatawazwa kuwa nyota wa mchezo, kwa kuthamini mchango wangu kuisaidia timu isipate kuruhusu bao lolote. Usiku wa siku hiyo, tukiwa tumejipumzisha kunako hoteli tuliyofikia ndani ya jiji la Dar- es- Salaam, nikampigia simu mpenzi wangu,ambaye nilikuwa naye katika mahusiano ya uchumba...huyu alikuwa akifahamika kwa jina la Vivian.

"Unaendeleaje, Vivian?"

"Naendelea vema tu...sijui wewe 'Shujaa' wangu..!?"

"Nipo salama, ndiyo tumetoka kwenye mechi jioni hii..!"

"Nimeangalia mechi leo, mpenzi..! Hongera sana kwa kucheza vizuri, laazizi..!". Aliniambia Vivian, akitumia sauti maridadi iliyokuwa imelegezwa vema kwa ufundi wa kike.

"Nashukuru, Mungu ametenda!". Nikasema hayo kudhihirisha ujuzi wa Mungu alionitunuku pamoja na kipaji makini. Nikamsikia akijichekesha kwa namna ya kudeka kwa dhahiri, nami nikaachia tabasamu usoni mwangu nikiwa nimeridhika mno.

Vivian alikuwa ndiye mwanamke niliyekuwa naye katika mahusiano ya uchumba. Tulikuwa tumefikia hatua ya kutambulishana hadi kwa wazazi na tayari tulivishana pete, kusubiri majaliwa ya Mwenyezi Mungu kuruhusu ndoto yetu ya kuwa mume na mke ipate kutimia.

"Enhe..!! Unarudi lini nyumbani..?". Aliniuliza Vivian.

"Hivi karibuni tu, mama. Tunasubiri neno kutoka kwa viongozi wa timu ndipo jambo lipate kufanyika...kama ni kurudi nyumbani au vinginevyo.".

"Lakini, si uliniambia kuwa ligi imekaribia kuisha?".

"Ndiyo, ligi imeisha. Lakini kuna jambo langu nalisubiri huku Dar- es- Salaam. Nafikiri nitabaki huku kwa siku kadhaa kusubiri kambi ya timu ivunjwe, halafu ndipo nikamilishe hilo suala.!".

"Kwani kuna nini unachotaka kufanya huko?"

"Ni masuala ya kikazi, mpenzi. Kwahiyo nitakueleza kila kitu kitakachojiri.". Nilimpa ukweli wote Vivian, kwa maana sikuwahi kufikiria kumdanganya kuhusu masuala yangu ya kikazi na hata alikuwa akiyafahamu vema baadhi ya mambo yangu ya kikazi. Tena, ikumbukwe kuwa, hakuwa msichana tu wa kuwa naye kwa ajili ya starehe za mwili ama kusogeza siku, bali aliandaliwa kuwa mke...na ndiyo maana nilipenda sana ayafahamu mengi kuhusu kazi yangu.

"Ahaaa,..! Sawa, mie wala sina neno. Isipokuwa tu, nakutakia kila la heri kwenye huo mchakato wako.".

"Usijali. Kila kitu kitakwenda katika mstari kama kawaida...na nitajitahidi kurudi nyumbani mapema sana...! Najua umenikumbuka sana, Vivian..!". Nilimwambia nikijitahidi kumtia moyo na kumbembeleza mrembo yule asijisikie vibaya. Nikamsikia akicheka kidogo, nami niiatabasamu...huiu nikiwa nina imani kuwa amenielewa na hawezi kuweka pingamizi lolote.

Tukayazungumza mengi kuhusu maisha yetu. Kubwa tu, alikuwa akinisisitiza nisijisahau nikalisaliti pendo lake kwa maana alikuwa akinipenda sana. Vivyo hivyo, nami pia sikubaki nyuma. Nikachukua nafasi ile muhimu kumtaka naye ajichunge na kujiheshimu, hata asipate kufungua milango kwa wafitini na walaghai kuharibu penzi. Hilo akanitoa wasiwasi kuwa tunda langu liko salama na amelitunza sana kunisubiri mimi tu.

*. *. *.

Maadamu ligi ilikuwa tayari imekwisha, na tayari timu yetu ilikuwa imekamilisha ratiba yote ya mechi zilizotakiwa kuchezwa, basi taarifa maalumu ya kuvunjwa kwa kambi na kuanza kwa kipindi cha mapumziko ikapata kutolewa rasmi kutoka kwa uongozi wa klabu ya nyumbani niliyokuwa nikiitumikia...timu ya Wajenzi FC. Basi, suala lililokuwepo ni wachezaji kurejea majumbani mwao kwa ajili ya kuendelea na maisha pamoja na familia zao. Mimi sikuwa na ratiba ya kurejea nyumbani Dodoma katika siku za karibuni baada tu ya kuisha kwa ligi kuu, na badala yake nikaingia rasmi katika mchakato wangu niliokuwa 'nikiupigia mahesabu'.

Suala la kwanza nikaamua kumtafuta wakala wangu ambaye alikuwa ndiye msimamizi wa mambo yangu binafsi ya kimikataba, kisheria, kimaslahi pamoja na kunitafutia masoko ya kujitangaza. Huyu, alikuwa ni kaka yangu wa damu kabisa, aliyekuwa ndiye aliyeniachia ziwa...Alex.

Basi, yakapangwa makutano na tukakutana kujadili suala hilo la usajili. Na akanijulisha kuwa palikuwepo na timu moja iliyokuwa ikicheza ligi kuu ya Tanzania Bara, iliyokuwa ikiitwa Namungo FC, iliyokuwa ikihitaji kuweka dau na kunisajili katika nyakati za dirisha kubwa la usajili, lililokuwa mbioni kufunguliwa rasmi baada ya

kumalizika kwa msimu wa kimashindano. Kwa wasiofahamu, dirisha la usajili ni soko ambalo hutambulika na Shirikisho la mpira wa miguu, ambalo huhusisha kuuzwa na kununuliwa kwa wachezaji, linalofunguliwa na kufungwa kulingana na kalenda ya Shirikisho.

Kwangu, zlilikuwa ni taarifa njema sana, kuona kwamba hatimaye kipaji changu kikipanda thamani hata timu tofauti zikianza kujitaji huduma yangu kama mchezaji. Kwa kiasi kikubwa, nilichukulia kama fursa ya kufika mbali zaidi, kwa maana pia timu ya Namungo FC ilikuwa ikishiriki mashindano ya kimataifa, kumaanisha kuwa huo ulikuwa wakati wangu mzuri pia kutimiza ndoto yangu ya kucheza mashindano hayo lakini pia nilitazama namna ambavyo milango ya kutoka na kwenda kucheza nje ya nchi ingefunguka kutoka hapo.

Kama haitoshi, tukafanya makutano na mmoja kati ya viongozi wa klabu ya Namungo FC, aliyekuwa mmoja kati ya wajumbe wa kamati kuu ya usajili. Makutano haya yalikuwa ya siri kwa maana bado nilikuwa nipo ndani ya mkataba uliokuwa ukinipa ajira ndani ya klabu ya Wajenzi FC kwa kipindi cha mwaka mmoja zaidi...hivyo kukutana na viongozi wa timu nyingine, tena kwa ajili ya masuala ya usajili hakika ingekuwa kinyume na taratibu na sheria. Naam...‼ Mazungumzo yakaenda vema na sasa makubaliano ya awali yakafikiwa baina yangu na klabu ya Namungo FC.

*. *. *.

Mara baada ya kuhitimishwa kwa makubaliano yale, nikapatiwa na fungu dogo la pesa kwa ajili ya matumizi binafsi kutoka kwa mjumbe yule, akinisisitiza sana nisije "kuwachiniia baharini' kwa maana walikuwa na nia ya dhati dhidi yangu na kama hilo halitoshi...walinihakikishia kupata nafasi ya kucheza katika kikosi cha kwanza haraka iwezekanavyo , pindi tu nitakapokubali kujiunga na timu yao.

Mimi pamoja na kaka yangu Alex, hatukuwa na mambo mengi zaidi, na tukajiondoa hotelini hapo mapema sana mara baada tu ya kumaliza mazungumzo yale. Tulifanya hivyo kwa sababu za kiusalama na za maadili ya kazi na ya kimikataba, kama jinsi nilivyopata kueleza hapo awali. Tulipotoka hapo, kituo kilichofuata kilikuwa ni nyumbani

kwa kaka yangu ambaye alikuwa akiishi pale pale Dar- es- Salaam kutokana majukukumu yake ya kikazi pamoja na biashara zake alizokuwa akiziendesha.

*. *. *.

Nikarejea nyumbani, ndani ya jiji la Dodoma kwa ajili ya mapumziko ya kumalizika kwa msimu wa kimashindano. Nikapata kufika nyumbani, kule nilipozaliwa na kukulia, nyumbani kwa Mzee Kasenga David. Kitendo cha kutia timu tu katika viunga vya mtaa ule, basi watu wengi walinilaki kwa bashasha tele na kunionesha matabasamu mapana. Wengi, walinisifu sana kwa kiwango changu kizuri nilichokionesha katika mechi nyingi ndani ya msimu huo uliomalizika. Wengine, wakanieleza kuwa walikuwa wakiifuatilia sana timu yetu ya Wajenzi FC, na ni kutokana na uwepo wangu katika timu ile...wakidai kuwa, nilikuwa ni sawa na 'nembo' ya mtaa wetu ndani ya nchi ya Tanzania.

Yote hayo waliyokuwa wakiniambia, yalikuwa yakinifariji sana na kujihisi kuwa ninalo deni kubwa la kuwalipa wadau wa soka pamoja na watu wa mtaani kwetu, kwa kuhakikisha ninapata mafanikio makubwa katika soka hata nikalitambulisha vema jina langu na la mtaa, pamoja na jina la jiji la Dodoma. Lakini, pia nilijihisi kuwa walau mimi pia ni sehemu ya jamii kwa namna ambavyo walikuwa wakinipenda na kunionesha kuwa baga kwa bega na mimi. Na ndiyo maana, siku hiyo niliacha gari langu nyumbani nilipokuwa nikiishi, kisha kufika mtaani hapo nikiwa natembea kwa miguu nikiwa na wafuasi kadhaa kando yangu.

Nilipofika nyumbani, nikapata mapokezi mema kama kawaida. Ndugu zangu, na hasa wadogo zangu ndiyo walikuwepo hapo, pamoja na baba na mama yangu. Nilikuta wamechinja beberu mmoja mkubwa kwa ajili ya kitoweo cha siku hiyo. Nyama zikapikwa na kukaangwa, huku nyingine zikichomwa kama mishikaki na nyama choma...nyama ikapata kuliwa 'kisawa sawa' ...!

Jambo lingine la kufurahisha na pengine la kipekee kabisa ambalo lilinikosha nafsi, ni kuhusu uwepo wa mchumba wangu Vivian, aliyefika kujiunga nami kwa ajili ya mapumziko yangu. Kwahiyo,

alipokuwa amefika, basi kila kitu kikawekwa sawa kwa ajili yetu. Palikuwepo na vyumba vipatavyo viwili vya kufikia wageni, hivyo mimi na Vivian tulipatiwa chumba kimoja ambacho tayari kilikuwa kimetayarishwa rasmi kabisa kwa ajili ya kuupokea ujio wetu pale nyumbani hapo.

Ndugu wengine pia nao wakipewa habari juu ya uwepo wangu nyumbani hapo. Wacha tu niseme, mimi Marco David... nilikuwa sawa na 'nuru' ya ukoo..! Nilikuwa nikipendwa sana na ndugu zangu, pengine ni kutokana na hali ya mimi kuwa mwanasoka anayevuma sana ndani ya nchi.

Kusema kweli, familia nyingi, na hasa hizi zinazopatikana ukanda wa Afrika pamoja na nchi nyingi zinazoendelea, ni kuwa wamejivika mazoea ya kumpenda sana mwanafamilia ama ndugu aliyefanikiwa kimaisha. Na pia wamekuwa na utaratibu wa kumtegemea katika kuwatimizia mahitaji yao. Nishukuru Mungu tu kuwa hali ilikuwa ni tofauti kidogo kwa upande wangu na ndugu zangu.

Kwahiyo, wengi waliozipata taarifa za ujio wangu nyumbani hapo waliishia kufurahi sana, huku wengi wakitoa ahadi ya kufika kwa lengo la kunisalimu na kunijulia hali.

*. *. *.

Nilikuwa nimejilaza kitandani, macho yangu yakimtazama Vivian ambaye alikuwa amerejea kutoka bafuni alipokwenda kufanya usafi wa mwili. Mwili wake maridhawa ulikuwa umestiriwa wa taulo moja tu lililokuwa likiishia juu kidogo ya magoti yake, nami nikapata wasaa mzuri wa kuyatazama mapaja manene ya rangi nyeupe asilia isiyochangamana na vipodozi vya kemikali. Miguu yake ilikuwa imejaa vema, watoto wa mjini wanaweza kusema kuwa Vivian alikuwa na 'mguu wa bia'. Nikameza funda la mate, nikishusha pumzi laini...kwa maana nilikuwa nikilitamani umbo lake kwa uchu.

Alipomaliza kujikausha maji mwilini mwake, alinisogelea na kuja kujiunga nami kitandani. Akapandisha mguu wake wa kwanza taratibu huku jicho lake la kichokozi likinitazama usoni. Paja lake likaonekana tena, na akapandisha mguu wa pili na tukawa wote kitandani. Akaja kunilalia kifuani kwa kunidekea kusiko semekana..! Bila shaka,

alikutana na kifua kilichojazwa nyama na kujengeka vema kutokana na mazoezi makali niliyokuwa nikifanya mara kwa mara kama mchezaji. Mkono wake ukanipapasa hadi chini ya kifua, nako pia palijengeka vema, maana tumbo langu lilikuwa limeimarika haswa na misuli yake ikajenga 'vifungu' vidogo vidogo, wenyewe wanaita 'six- packs'. Akautembeza mkono wake maeneo hayo kwa sekunde kadhaa. Kutokana na ulaini wa mkono wake, nakjihisi raha sana..!!

"Marco... Nilikumisi sana mpenzi wangu..!!" ...nilimsikia akiniongelesha kwa sauti ya chini kabisa. Kisha akakibusu kifua changu alichokifanya kuwa mto wa kulalia. Ule msisimko wake, haukuwa na kifani. Nami sikubaki nyuma, nikakipapasa kiuno chake hadi nikazisalimu na hipsi zake za wastani, nikahisi mtikisiko wa kiuno chake kidogo, akaisogeza sura yake na kunidai kutano la kinywa kwa kinywa, nami sikuwa na hiyana...nikampatia kwa utimamu wake.

"Sidhani kama unanizidi... sijui hata ningekuwa wapi muda huu kama nisingerudi nyumbani, sijui kama ligi ingekuwa inaendelea,...!!"...akaniwahi kabla sijaimaliza hii sentensi, kwa kuniwekea kidole chake mdomoni mwangu, ishara ya kutaka nikae kimya. Kisha akatawala tena mazungumzo yetu.

"Unapokuwa na mimi, sihitaji uzungumze kuhusu masuala yako ya kazi, hadi nitakapokupa ruhusa. Sasa upo kifungoni, uko chini ya jela yangu...na utatumikia kifungo changu ipasavyo..sawa..!?". Nikakosa hata la kusema, kidume mzima nikatii amri kwa kidole chake tu..!! Baada ya kuyasema hayo, nikamuona akitabasamu tena hata nikauona mwanya wake. Akanikaribisha katika 'jela' yake na kunitia 'pingu' na nikatii. Tukafungamana kihisia na tukajiosa rasmi katika bahari ya mapenzi.